

رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِينَ

Shukurani zote zamhusu Mwenyezi Mungu  
kwamba sawa na haja ya wakati,  
kwa kuwaokoa wengi katika tauni,  
kijitabu hiki kimeandikwa,  
na jina lake ni

# **KINGA YA BALAA NA KIPIMO CHA WATEULE**

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian  
Masihi Aliyehadiwa na Imam Mahdi<sup>as</sup>

Mfasiri

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

*Kinga ya Balaa*

Tafsiri ya Kiswahili ya *Dāfe‘ul Balā*

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1902

Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2009

Nakala: 3000

Kimeenezwa na:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania

Mnazi mmoja, Dar es Salam.

Simu: +255222110473

Fax: +255222121744

Kimechapwa na:

Ahmadiyya Printing Press

Dar es Salam, Tanzania

Simu: +255222111031

ISBN: 9987 - 438 - 11 - 3

# Faharisi

<i>Yaliyomo</i>	<i>Kurasa</i>
Maelezo ya Mwenezi	5
Tanbihi	7
Hadhrat Isa <sup>as</sup> alikuwa mwema	8
Tauni	11
Njia mbali mbali za kusalimika na tauni	11
Ahadi za Mungu kuisalimisha Qadian	17
Mungu hana mwana	20
Habari ya tauni katika funuo za Seyyidna Ahmad <sup>sa</sup>	22
Yalindeni Makao yenu	24
Maombi ya Makafiri hayakubaliwi	27
Enyi Wahubiri wa Kikristo	28
Enyi Mashia	29
Kifo cha nabi Isa <sup>as</sup>	32
Maana ya kufunga kwa Mungu	36
Ishara yangu	37
Habari kwa watu wote	39
Mbora kuliko Yesu	42
Nimekuja pamoja na Maelfu ya Malaika	44
Nyongeza nambari 1	46
Nyongeza nambari 2	47





## Maelezo ya Mwenezi

Naona furaha sana kuweka mbele ya wasomaji tafsiri hii ya kitabu cha Seyyidna Ahmad<sup>as</sup>, mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kiitwacho '*Dāfe 'ul Balā'*, Kinga Ya Balaa. Kitabu hicho kilichapishwa katika Aprili 1902, wakati tauni ilipoenea sana katika mkoa wa Panjab nchini India.

Katika kitabu hiki Seyyidna Ahmad<sup>as</sup> ameeleza funuo zake kuhusu kuenea kwa tauni na sababu zake kwamba Masihi aliyetumwa na Mungu siyo alikataliwa pekee bali aliudhiwa, hila zilipangwa kumwua na aliitwa kafiri na dajali.

Wakati ule Seyyidna Ahmad<sup>as</sup> alitabiri kwamba yeye na makao makuu yake, Qadian, yatalindwa na tauni na wengine hawataweza hata kutangaza kuhusu usalama wao na wa makao yao katika maangamizo ya tauni.

Alitangza sawa na ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

"Katika kila hali, maadamu tauni ipo duniani, hata kama iwepo kwa miaka sabini, Mwenyezi Mungu Atahifadhi Qadian katika maangamizo yake ya kuogofya" (uk24).

Na akaandika:

"Ishara yangu ndiyo hii kwamba kila mpinzani hata akikaa huko Amroha au Amritsar au Delhi au Kalkata au Lahore au Golra au Batala, kama atasema kwa kuapa kwamba mahali pake fulani patasalimika na

tauni, basi lazima kabisa mahali hapo patashikwa na tauni, kwani amekosa adabu mbele ya Mwenyezi Mungu". (uk37)

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri wa zamani wa Kenya, Tanzania na Ghana. Na tafsiri hii ilipitiwa na Sheikh Mubarak Mahmud katika '*Deski ya Kiswahili*', Rabwah. Kisha Maulana Sheikh Jamil-ur-Rahman Rafiq aliiboresha kwa ustadi mkubwa na kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana.

Aidha, ndugu kadha wengine nao wakasaidia katika kukamilisha kazi hii, kama vile Sheikh Ansar Husain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal, na Sharifu Tanwir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.

Wakilut Tasnif

Tahrike Jadid.

Rabwah, Pakistan.

22 Juni 2009.

# Tanbihi

Ujumbe tunaopenda wakati huu kuwafikishia wananchi wapenzi kwa njia ya kijitabu hiki, kuhusu huo imethibitika kutokana na tajiriba ya zamani ya Manabii<sup>as</sup> kwamba kwa sasa hivi huruma yetu hii itathaminiwa kwa njia hii tu kwamba mara nyingine tena tutasikia matusi na tutatajwa kwa majina ya namna namna ya kuudhi kutoka kwa masheikh wa Islamu na mapadre wa Kikristo na mapandati wa Kibaniani. Na tunajua sana mapema kwamba itakuwa hivyo tu, lakini tumetanguliza kuwahurumia wanadamu juu ya kuudhiwa na midomo michafu ya watu wote; kwani juu ya hayo inawezekana pia kwamba miongoni mwa hao mamia na maelfu ya wanaotusi, wapatikane wengine katika wakati uteremkapo moto toka mbinguni – bali katika kipupwe kijacho inatazamiwa kuteremka zaidi – ambao watasoma kwa makini kijitabu hiki na hawatamkasirikia haraka nasiha wao huyu mwenye huruma na watajaribu njia niwaambiayo. Maana, hawakutakiwa kutoa ujira au malipo yoyote badala ya huruma hiyo. Kwa ikhlasi ya kweli tu na nia njema, shauri moja njema iliyokwisha jaribiwa imetolewa kwa kuwaokoa wanadamu. Basi, ikiwa watu katika maradhi wanakunywa hata mkojo wa baadhi ya wanayama na kutumia vitu vingi vichafu, basi katika hali hii wana shida gani

kujichagulia tiba hii safi ili kujiokoa. Na kama hawatafanya, hata hivyo kwa vyovyote watatambua siku moja katika wakati wa shindano kwamba miongoni mwa dini hizo zote ni dini gani inayoweza kuthibitika kuwa mwombezi na kuwa uthibitiko wa neno kubwa la "mwokozi". Kila mtu anataka mwokozi wa kweli na anampenda. Basi, bila shaka sasa siku zimefika za kuthibitika kwamba mwokozi wa kweli yu nani? Sisi bila shaka tunamtambua Masihi mwana wa Mariamu kuwa mtu mkweli kwamba alikuwa mwema kuliko watu wengi<sup>1</sup> wa

---

<sup>1</sup> Ikumbukwe kwamba tuliyosema kuwa Hadhrat Isa<sup>as</sup> alikuwa mwema kuliko watu wengi wa zama zake, kauli yetu hii ni kama dhana tu njema, waila inawezekana kwamba katika zama za Hadhrat Isa<sup>as</sup>. Pengine katika ardhi ya Mwenyezi Mungu baadhi ya wakweli walikuwa bora na watukufu zaidi katika ukweli na uhusiano wao na Mungu kuliko Hadhrat Isa<sup>as</sup>. Maana, Mwenyezi Mungu kuhusu yeye Amesema: **وَجِئْنَا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمِنَ الْمَثَرِينَ** (Mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu miongoni mwa waliokaribishwa. Aali-Imran:46)

Hiyo inamaanisha kwamba yeye naye alikuwa mmojawapo miongoni mwa waliomkurubia Mungu katika zama zile. Haithibitiki kwa hiyo kwamba yeye alikuwa amewazidi wote waliomkurubia Mungu, bali upo uwezekano wa jambo hili kwamba baadhi ya waliomkurubia Mungu katika zama zake walikuwa bora kuliko yeye. Ni dhahiri kwamba yeye alikuja kwa kondoo wa Wana wa Israeli tu, na hakuhusiana hata kidogo na nchi zingine na mataifa mengine. Basi yumkini bali yaelekea sana kwamba baadhi ya manabii walikuwa bora na aula kuliko yeye ambao wamo katika wale waliotajwa katika: **لَتَنْقُضُوا** (Hatukukusimulia. Al-Mumin:79)

Na kama vile dhidi ya Hadhrat Musa<sup>as</sup> hatimaye mtu mmoja akatokea, ambaye kumhusu yeye Mungu Amesema: **عَلَّمْنَاهُ مِنَ لَدُنَّا عِلْمًا** (Tukamfundisha elimu kutoka Kwetu. Al-Kahf:66)

zama zake. Na Mungu ndiye Ajuaya sana. Lakini yeye hakuwa mwokozi wa kweli. Yuasingiziwa kwamba alikuwa mwokozi kwa hakika. Mwokozi wa

---

<sup>2</sup>basi tunawezaje kusema kumhusu Hadhrat Isa<sup>as</sup> ambaye alikuwa mdogo sana kuliko Musa<sup>as</sup> na alikuwa mfuasi wa sheria yake na mwenyewe hakuleta sheria kamili, na alikuwa chini ya sheria ya Hadhrat Musa<sup>as</sup> katika mambo ya tohara na masa'ala za fikih na urithi na uharamu wa nguruwe na kadhalika, kwamba yeye kwa ujumla alikuwa amewapita wakweli wote wa zama zake? Wale waliomfanya yeye kuwa Mungu kama Wakrisito, au wale ambao wamempachika pasipo msingi sifa za Uungu kama vile wapinzani wetu na wapinzani wa Mungu, Waislamu wa jina, hao kama wakiendelea kumnyanyua, wampandishe mbinguni au wamkalishe juu ya Arshi au wamchukulie kuwa mwumbaji wa ndege kama Mungu, basi wana hiari. Mtu akiacha haya na uadilifu, hapo aseme apendavyo na afanye atakavyo; lakini unyofu wa Yesu hauthibitiki zaidi kuliko wanyofu wengine wa zama zake. Bali Nabii Yahya anayo fadhila moja juu yake, kwani alikuwa hatumii ulevi wala haikusikika kwamba mwanamke mmoja mwasherati akaja na uturi alionunua kwa fedha alizojichumia na akaupaka kichwani mwake; au aliugusa mwili wake kwa mikono na kuupangusa kwa nywele za kichwa chake; au mwanamke kijana asiyehusika akamtumikia. Kwa sababu hiyo Mungu Alimwita Yahya katika Kurani jina Hasur حُصُورًا\* (mtawa). Lakini hakumwita Yesu jina hilo, kwani visa vya aina hiyo vilizuia asiitwe jina hilo. Na tena Hadhrat Isa<sup>as</sup> alitubu dhambi zake kwa mkono wa Hadhrat Yahya na akaingia katika wafuasi wake mahususi, ambaye Wakristo wanamwita Yohana ambaye baadaye akafanywa Eliya. Na jambo hili linathibitisha kwa uwazi ubora wa Hadhrat Yahya, kwani kinyume chake haikuthibitishwa kwamba Yahya pia alitubu kwa mkono wa yeyote mwingine. Basi kuwa kwake maasumu ni jambo la wazi kabisa. Na habari hii iliyoenea baina ya Waislamu kwamba Isa<sup>as</sup> na mamake hawakuguswa na Shetani, hawaelewi watu wajinga maana yake. Hakika yenyewe ni kwamba Mayahudi waovu walimsingizia Hadhrat Isa<sup>as</sup> na mamake kwa masingizio machafu sana, na kuhusu wote wawili hao, Mungu Atupishe mbali, walituhumu kuwa wakatenda matendo ya Kishetani. Kwa hiyo ilikuwa hakuna budi kukanusha masingizio hayo. Basi, Hadithi hii haina maana zaidi ya haya kwamba masingizio hayo machafu aliyosingiziwa Hadhrat Isa<sup>as</sup> na mamake siyo sahihi. Bali kwa

kweli mwenye kuokoa daima dawamu na mpaka Kiama ni yule aliyezaliwa katika nchi ya Hijazi, na aliyekuja kwa kuokoa dunia yote na zama zote, na sasa tena amekuja lakini kwa namna ya mfano. Mungu Ainufaishe ardhi nzima kwa baraka zake. Amin.

Mnyenyekevu,  
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

---

maana hii, hao hawakuguswa na Shetani; na nabii mwingine yeyote hakuikabili hali ya namna hiyo ya kuondolewa masingizio. Mwandishi.

\*(Aali-Imran: 40)

---

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ<sup>3</sup>  
نُحَمِّدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ<sup>4</sup>

## Tauni

(Tafsiri ya beti za Kiajemi)

*Maadamu tauni imekuja toka kwa Mungu, uitazame kwa jicho la heshima. Ewe fasiki, wewe ndiwe maluuni, kwa nini unaiita hiyo maluuni?*

*Hizi ni zama za toba na wakati wa kujisahihisha na kuacha uovu.*

*Mtu ashikiliaye bado uovu, sioni mwisho wake kuwa mema.*

Kuhusu ugonjwa huu wa kutisha unaoendelea kuenea nchini, watu wana maoni tofauti. Madaktari ambao fikira zao zinaishia kwenye tadbiri za kimwili tu, wanasisitiza kwamba wadudu fulani wamezalika ardhini kwa sababu za kiasili, ambao kwanza wawaathiri vibaya panya,<sup>5</sup> kisha katika wanadamu vifo vinafululiza kutokea. Na ugonjwa huu

---

<sup>3</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

<sup>4</sup> Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume Wake Mtukufu<sup>sa</sup>

<sup>5</sup> Sawa na kanuni za utabibu yalizimu kwa kutambua ugonjwa wa tauni kwamba katika kijiji au mji wenye bahati mbaya, au katika sehemu yake yoyote ugonjwa huu uangamizao ukienea, panya waliokufa wapatikane siku kadha hapo kabla. Basi, kwa mfano, kama katika kijiji fulani vifo vichache vitokee kwa homa na panya wasionekane wakifa, basi hiyo siyo tauni, bali ni homa iangamizayo aina ya taifodi. (Mwandishi).

hauhusikani na fikara za kidini, bali inapaswa kulinda nyumba na miferiji katika takataka za kila aina na uvundo na kuviweka safi na kuendelea kuvitakasa kwa nafthalini (dawa ya kuua wadudu), na kuwasha moto katika nyumba kwa kuiweka katika hali ya joto-joto, na kuifanya ipitiwe na hewa na mwanga pia. Na katika nyumba yoyote wasikae watu wengi isije kwa pumzi zao na kwa kinyesi na mkojo na kadhalika wadudu wakapata kuzalika. Wasile vyakula vibovu. Na tiba bora zaidi ni kwamba wadungwe sindano. Na kama wakiona nyumbani panya waliokufa, basi waziache nyumba hizo. Afadhali wakae nje viwanjani, na wajiepushe na nguo chafu. Na kama mtu akija katika mji wao au kijiji chao kutoka katika nyumba iliyoathirika na kuingiziwa na ugonjwa basi wasimruhusu kuingia ndani. Na kama mtu wa kijiji au mji huo augue maradhi hayo, basi wantoe nje na wajiepushe na kuchanganika naye. Basi, sawa na maoni yao tiba ya tauni ndiyo hiyo tu. Hiyo ndiyo rai ya madaktari wenye busara na matabibu ambayo hatuioni kwamba ni tiba ya kutosha na ya kudumu wala hatusemi kuwa haina faida katu. Hatuioni ni tiba ya kutosha na kudumu kwa sababu tajiriba inathibitisha kwamba baadhi ya watu walikufa, ingawa walitoka nje. Na baadhi yao wakiendelea kushikamana na usafi wakaaga dunia hii, na baadhi yao wakapigwa sindano kwa tumaini sana lakini wakaingia kaburini. Basi, nani anaweza kusema au

nani anaweza kututuliza kwamba tadbiri hizo zote ni tiba ya kutosha. Bali twalazimika kukiri kwamba ingawa njia hizo zote zina faida kiasi fulani, lakini tadbiri hiyo siyo ambayo twaweza kusema kwamba ni ufaulu kamili kwa kuondolea mbali tauni nchini.

Kadhalika, tadbiri hizo pia si bure tu, kwani popote pale Mungu apendapo faida yake pia inaonekana hapo, lakini faida ile hairidhishi sana. Kwa mfano, ingawa ni kweli kwamba kama watu mia moja wamedungwa sindano na watu wengine kiasi hicho hicho hawakudungwa sindano; wale ambao hawakudungwa sindano kati yao vifo vingi vimetokea, na kati ya waliodungwa sindano vimetokea vichache. Lakini, kwa kuwa athari ya sindano ndiyo hadi miezi miwili au mitatu, kwa hiyo mwenye kupigwa sindano pia ataingia hatarini mara kwa mara mpaka aondoke dunia hii. Tofauti ni hii tu kwamba wasiodungwa sindano wamepanda farasi ambaye, kwa mfano, anaweza kuwafikisha kwenye mauti katika masaa ishirini na manne; na wale wanaopigwa sindano wamepanda aina ya farasi mfupi, mzito wa mwendo ambaye atawafikisha pale pale katika siku ishirini na nne. Kwa vyovyote, njia hizo zote zilizochaguliwa kiudaktari, hazitoshi wala haziridhishi kikamilifu, na pia si bure kabisa au bila faida. Na kwa kuwa tauni inaimeza nchi haraka haraka, hivyo huruma ya binadamu yataka ifikiriwe njia nyingine, iwezayo kulinda katika maangamizo haya.

Na Waislamu wanasisitiza, kama vile inavyofahamika kutoka katika tangazo la Mian Shamsuddin, Katibu wa Anjuman Himayati Islam Lahore, alilotoa mwezi huu, yaani Aprili 1902, kwamba madhehebu yote ya Waislamu, Washia, Masuni, wafuasi wa maimamu na wasiokuwa wafuasi, wakienda nyanjani, wafanye maombi sawa na njia ya madhehebu yao na wasali wakijumuika tarehe hiyo hiyo moja. Basi hii ndiyo njia ambayo kwayo tauni itaondoka papo hapo. Lakini, watajumuikaje, haijaelezwa njia yake. Ni wazi kwamba sawa na imani ya dhehebu la Wahabi (Ansar Suna) sala haisihi bila kusoma sura Fatiha; katika hali hii sala ya Wahanafi inawezekanaje pamoja nao? Je hautatokea ufiisadi baina yao? Zaidi ya hayo, mwandishi wa tangazo hilo hakueleza kwamba Mabaniani wafanye nini kuondoa maradhi hayo. Je, wanayo ruhusa au hapana kwamba wao nao wayaombe masanamu yao msaada wakati huu? Na Wakirsto washike njia gani? Na madhehebu ambayo wafuasi wake wanamwaamini Hadhrat Husain<sup>ra</sup> au Hadhrat Ali<sup>ra</sup> kuwa wenye kutimiza mahitaji, na katika Muharamu<sup>6</sup> wanapeleka maelfu ya maombi

---

<sup>6</sup> Huu mwezi wa Muharamu ni wenye baraka sana. Kuhusu fadhila yake Hadithi ya Mtume Mtukufu<sup>sa</sup> imeandikwa katika "Tirmidhi" kwamba فِيهِ يَوْمٌ تَابَ اللَّهُ فِيهِ عَلَى قَوْمٍ وَيَتُوبُ فِيهِ عَلَى قَوْمٍ آخَرِينَ Yaani, katika Muharamu kuna siku moja ambamo Mungu Aliwaokoa watu katika balaa katika zama zilizopita, na imepangwa kwamba katika mwezi huo huo watu wengine nao wataokolewa

kwa kupata miradi yao kwenye vigezo vya ziara la Imam Husain wanavyotoa katika maandamano, au Waislamu ambao wanamwabudu Sayyid Abdul Kadir Jilani au wanamwabudu Shah Madari au Sakhii Sarwari wafanye nini. Na je, wafuasi wa madhehebu hayo yote hivi sasa hawaombi? Bali kila dhehebu kwa kushikwa na hofu linamwita Mwabudiwa wake.

Piteni katika mitaa ya Washia, hakutakuwa na nyumba isiyoandikiwa mlangoni pake ubeti huu:

لِيْ خَمْسَةٌ أُطْفِيْ بِهَا حَرَّ الْوَبَاءِ الْحَاظِمَةِ الْمُضْطَّرِّ وَالْمُرْتَضَىٰ وَابْنَاهُمَا وَالْفَاطِمَةَ<sup>7</sup>

Mwalimu wangu alikuwa mzee mmoja Mshia, yeye alikuwa akisema kwamba tiba ya maradhi ya kuambukiza ni *Tawalla* na *Tabarra* tu, Yaani, kuwapenda maimamu wanaotokana na wazao wa Mtume<sup>sa</sup> sana mno kiasi cha kuwaabudu, na kudumu kuwatusi masahaba<sup>ra</sup>, hakuna tiba bora zaidi kuliko hii. Nami nimepata kusikia kwamba huko Bombay tauni ilipoanzia, awali fikira ilizuka baina ya watu kwamba huu ni mwujiza wa Imam Husain, kwani Mabaniani waliozozana na Washia, tauni ilizuka baina yao. Kisha maradhi hayo yalipowaingilia Washia pia, hapo kelele za "Ya Husain" zikapotea.

---

katika balaa moja. Si ajabu, balaa hilo liwe ni tauni, na kwa kumtii aliyetumwa na Mungu, balaa hili liondoke katika nchi. (Mwandishi)

<sup>7</sup> Ninao waja watano ambao kwao napoza hari ya maradhi ya kuambukiza yanayoangamiza, nao ndio: Muhammad Mustafa<sup>sa</sup>, Ali Murtadha<sup>ra</sup> na wanao wawili na Fatima<sup>ra</sup>

Hizo ndizo fikira za Waislamu zilizofikiriwa ili kuondoa tauni. Na kwa kudhihirisha fikira za Wakristo, sasa hivi limetolewa tangazo moja na Padre White Breakht na chama chake, nalo ndilo kwamba kuondoa tauni tadbiri yoyote haitoshi, isipokuwa tu kumwamini Yesu kuwa Mungu na kuiamini kafara yake.

Na miongoni mwa Mabaniani, wafuasi wa dhehebu la Aria wanasema kwa kupaza sauti kwamba balaa hili la tauni limesababishwa na kuacha Veda (Kitabu chao Kitakatifu). Madhehebu yote yanapaswa kuamini mafundisho ya Veda, na kuwahesabu Manabii wote kuwa wazushi, Mungu atupishe mbali, ndipo kwa njia hii tauni itaondoka.

Na dhehebu la Sanatan ambalo li miongoni mwa Mabaniani, katika dhehebu hili rai iliyodhihirishwa kuondolea mbali tauni, ambayo kama tusingesoma gazeti la "Akhbar-e-Aam" pengine tusingejua rai hii ya ajabu. Na rai ile ndiyo hii kwamba balaa la tauni limetokea kwa sababu ya ng'ombe. Kama serikali ipitishke kanuni hii kwamba katika nchi hii ng'ombe asichinjwe kabisa kabisa, ndipo mwone jinsi tauni inavyoondoka. Bali katika gazeti hilo hilo katika sehemu moja imeandikwa kwamba mtu mmoja alimsikia ng'ombe akizungumza na kusema kwamba kwa sababu yangu tu tauni imetokea katika nchi hii.

Sasa enyi wasomaji! fikirini wenyewe kwamba miongoni mwa kauli na madai tofauti kiasi hiki, kauli gani inaweza kukubaliwa kwa uwazi mbele ya dunia.

Hayo yote ni mambo ya kiitikadi na katika wakati huu wa hatari, mpaka dunia iamue kuhusu itikadi hizo, dunia yenyewe itahukumiwa. Hivyo, jambo lile linapaswa kukubaliwa linaloweza kueleweka haraka sana na lilio na uhakikisho pamoja nalo. Basi, naeleza jambo lile pamoja na uhakikisho. Miaka minne imepita nilipochapisha utabiri mmoja kwamba mkoani Panjab tauni kali itatokea. Nikaona (katika kashfi) nchini humu miti myeusi ya tauni iliyopandwa katika kila mji na kijiji. Kama watu wakitubu, maradhi hayo hayawezi kuendelea zaidi ya vipupwe viwili, Mungu Atayaondoa. Lakini badala ya kutubu nikatukanwa na yalichapishwa matangazo ya kunitusi. Matokeo yake ni hali hii ya tauni mnayoiona sasa. Wahyi mtakatifu wa Mungu ulioniteremkia maneno yake ni haya **إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ إِنَّهُ أَوَىٰ الْقُرَيَّةَ** Yaani, Mungu amenuia kwamba Hataliondoa kamwe balaa hili la tauni mpaka watu waondolee mbali fikira zile zilizomo miyoni mwao, yaani hadi wamkubali Mjumbe na Mtume wa Mungu, tauni haitaondoka. Na Mungu Mweza Huyu Atalinda Qadian na maangamizo ya tauni<sup>8</sup> ili mwelewe kwamba Qadian

---

<sup>8</sup> *Aawaa*, ni neno la Kiarabu, maana yake ni kulinda na maangamizo na tawanyiko na kuweka katika hifadhi yake. Hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba miongoni mwa aina za tauni, ile ndiyo yenye kuangamiza sana inayoitwa tauni *Jarif*, yaani yenye kufagilia mbali ambayo watu wanaikimbia huko na kuko, na wanakufa kama mbwa; hali hii inazidi kuvumiliwa na binadamu. Basi, katika maneno hayo ya Mungu imeahidiwa

ilihifadhiwa kwa sababu ya kuwepo Mtume na Mjumbe wa Mungu katika Qadian. Sasa tazameni, yaendelea kuthibitika tangu miaka mitatu kwamba pande hizo zote mbili zimetimia, yaani upande mmoja katika Panjab nzima tauni imeenea na upande mwingine, ingawa pande zote nne pembeni mwa Qadian, kwenye umbali wa maili mbili, tauni inaendelea kuzidi lakini Qadian haina tauni katu. Bali mpaka leo mtu yeyote aliyeshikwa na tauni, alipokuja Qadian toka nje, yeye naye akapona. Je, waweza kuwa uhakikisho wowote zaidi ya huu kwamba mambo yaliyosemwa miaka minne mapema tangu leo yamekwishatimia. Bali utabiri wa tauni ulitolewa

---

kwamba hali hiyo haitaisibu kamwe Qadian. Hiyo ndiyo imefafanuliwa katika ufunuo huu wa pili **لَوْلَا الْإِحْرَامُ لَهْلَكَ الْمَقَامُ**

Yaani, kama nisingejali heshima ya Jumuiya hii, ningehilikisha Qadian pia. Kwa ufunuo huu mambo mawili yanaeleweka. (1) La kwanza, haidhuru kama tukio lolote litukie kwa nadra katika Qadian pia kiasi cha kuvumiliwa na binadamu ambalo lisiwe la kuangamiza na kuwakimbiza watu na kuwasambaratisha; kwani kitu cha nadra ni kama kisichokuwepo. (2) La pili, ni kwamba katika vijiji na miji ambamo kulingana na Qadian wakaidi wakali, wakorofi, wadhalimu, waovu, wafisadi na maadui wakali wa Jumuiya hii wanaishi, hakuna budi tauni ya kuangamiza itazuka katika miji na vijiji vyao hata kwamba watu watakimbia kila upande kwa kupotewa na fahamu. Tumekwisha eleza maana hizo za *aawaa* sawa na upana wake. Nasi twaandika kwa uthabiti kwamba katika Qadian tauni iangamizayo haitaenea kamwe ambayo huwa yenye kuangamiza kijiji na kukimeza. Lakini kinyume chake katika miji na vijiji vingine vilivyo na dhuluma na ufisadi lazima zitatokea hali za kuogofya. Katika dunia nzima ni Qadian pekee iliyotolewa ahadi hiyo, kwa hiyo, basi, twamhimidi Mungu. (Mwandishi)

miaka ishirini na miwili tangu leo katika *Barahine Ahmadiyya*.<sup>9</sup> Na elimu hii ya mambo ya ghaibu, haimo katika uwezo wa mwingine yeyote isipokuwa Mungu. Basi, kwa kuondoa maradhi haya, ujumbe Alionipatia Mungu ndio huu kwamba watu waniamini kuwa Masihi Mau'udi kwa mioyo safi. Kama mimi nigefanya madai matupu bila dalili yoyote kama alivyofanya Mian Shamsuddin, Katibu wa Himayate Islam Lahore, katika tangazo lake au Padre White Breakht alivyofanya katika tangazo lake, hapo mimi nami ningekuwa mpayukaji kama hao. Lakini maneno yangu ndiyo niliyoyaeleza hapo kabla ya wakati na leo yamekwishatimia. Na kisha baadaye katika siku hizi pia Mungu Amenipatia habari. Huyo Mwenye nguvu na Jalali Anasema:

---

<sup>9</sup>Miaka kumi kabla ya leo katika kijitabu cha chanikiwiti nilichochapisha, utabiri kuhusu tauni ulitolewa, nao ndio huu:

إِصْنَعِ الْفَلَكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ

Yaani, tengeneza safina moja kwa amri yangu na mbele ya macho yangu, itakayolinda katika tauni itakayozuka. Watu ambao wanafungamana nawe kwa hakika wanafungamana nami. Huu sio mkono wako bali ni Mkono Wangu unaowekwa juu ya mikono yao. Na fungu moja la maneno hayo ya Mungu limo katika Barahine Ahmadiyya kama kiutabiri, nalo ndilo hili:

وَلَا تُخَاطِبُنِي فِي الدِّينِ عَلَّمُوا أَنَّهُمْ مُعْرِفُونَ Yaani, watu ambao hawatangani na dhuluma, uhalifu uovu na uasi, usiwaombe mbele yangu, kwani wataangamizwa. (Mwandishi)

مَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ. إِنَّهٗ أَوَى الْفِرْيَةَ . لَوْلَا الْإِكْرَامُ لَهْلَكَ الْمَقَامُ. إِنِّي أَنَا الرَّحْمَنُ دَافِعُ الْأَذَى. إِنِّي لَا يَخَافُ لَدَيَّ الْمُرْسَلُونَ. إِنِّي حَفِيطٌ. إِنِّي مَعَ الرَّسُولِ أَقْوَمُ. الْيَوْمَ مِنْ يَلُومُ. أَفْطِرُ وَأَصُومُ. غَضِبْتُ غَضَبًا شَدِيدًا. الْأَمْرَاضُ تُشَاعُ . وَالنُّفُوسُ تُضَاعُ . إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ . أُولَئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ . إِنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا. إِنِّي أَجْهَرُ الْجَيْشِ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَائِعِينَ . سُنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْأَفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ نَضْرَمِنَ اللَّهُ وَفَتَحَ مُبِينٌ. إِنِّي بَايَعْتُكَ بِابِعِي رَبِّي. أَنْتَ مِنِّي بِمَنْزِلَةِ أَوْلَادِي . أَنْتَ مِنِّي وَأَنَا مِنْكَ . عَسَى أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَحْمُودًا. الْفُوقُ مَعَكَ وَالتَّحْتُ مَعَ أَعْدَائِكَ . فَاصْبِرْ حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ . يَأْتِي عَلَى جَهَنَّمَ زَمَانٌ لَيْسَ فِيهَا أَحَدٌ<sup>10</sup>

<sup>10</sup> Kumbukeni kwamba Mwenyezi Mungu Hana wana, Hana mshirika wake wala Hana mwana, wala yeyote hana haki ya kusema kwamba mimi ni Mungu au mwana wa Mungu. Lakini hapa maneno haya ni kama majazi na istiyara. Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu Ametaja Mtume Mtukufu<sup>sa</sup> kuwa mkono wake, na Akasema:

يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ<sup>١١</sup> (Mkono wa Mwenyezi Mungu juu ya mikono yao. Al-Fat'ha:11). Kadhalika, badala ya kunena: "Sema, enyi watumishi wa Mungu", Akanena: "Sema, enyi watumishi wangu".

Na Akasema pia: فَالَّذِينَ كَفَرُوا وَاللَّهُ كَذِبُكُمْ أَبَاءَكُمْ (Basi Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu. Al-Baqara: 201)

Basi, someni Neno la Mungu kwa makini na uangalifu na liaminini kama aina ya *Mutashabihati*. Wala msiingilie katika maelezo yake, na uhakika wake ulivyo Mwachieni Mungu. Na muwe na yakini kwamba Mungu Ameepakana na kupanga mwana, ingawa kwa sura ya *Mutashabihati* yapo mengi katika Neno lake. Basi, mjiepushe na kufuata *Mutashabihati* na kuangamia. Na kunihusu mimi kuna ufunuo huu ulio miongoni mwa maneno yaliyo bayana, ulioandikwa katika *Barahine Ahmadiyya*: قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُؤْتِي إِلَهَ أَعْمَالِكُمُ إِلَهٌ وَاحِدٌ وَالْحَبِيرُ بِيَدِهِ الْقُرْآنُ (Mwandishi).

(Sema: Bila shaka mimi ni binadamu kama nyinyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, na heri zote zimo ndani ya Kurani Tukufu. Mfasiri)

Tafsiri: Mungu si Mwenye kuwaadhibu watu wa Qadian ilhali unakaa baina yao. Yeye Atakilinda kijiji hiki na uharibifu wa tauni na maangamizo yake. Kama nisingekujali wewe na kama nisingeangalia heshima yako, basi ningeangamiza kijiji hiki. Mimi ndimi Rahmani Mwenye kuondoa udhia. Mitume wangu hawana hofu katu mbele yangu wala huzuni. Mimi ni Mwangalizi. Nitasimama pamoja na Mtume Wangu, na Nitamlaumu anayemlaumu Mtume wangu. Nitagawa nyakati zangu; sehemu fulani ya mwaka nitafuturu, yaani Nitawaangamiza watu kwa tauni, na sehemu fulani ya mwaka nitafunga, yaani amani itakuwepo na tauni itapungua au itakwisha kabisa. Ghadhabu yangu inawaka; maradhi yataenea na maisha yatapotea, lakini watakaoamini pasipokuwa na ila katika imani yao watakuwa na amani na watapata njia ya kusalimika. Msidhani wahalifu wako salama, twaisogelea ardhi yao. Ninatayarisha jeshi langu ndani kwa ndani, yaani nawalea vijidudu vya tauni. Kwa hiyo, watajifia nyumbani mwao jinsi ngamia afavyo. Kwanza tutawaonyesha ishara zetu katika watu wa mbali, kisha ndani mwao wenyewe ishara zetu zitadhihirika. Siku zile zitakuwa za msaada wa Mungu na ushindi. Nimefanya biasahara nawe; yaani, kitu kimoja kilikuwa Changu ambacho ukafanywa mmiliki wake, na kitu kimoja kilikuwa chako ambacho Nikawa mmiliki Wake. Wewe nawe ukiri biashara hii

ukaseme Mungu Amefanya biashara nami. U kwangu kama wazao. Unatokana nami, Nami Natokana nawe. Wakati u karibu nitakapokupatia daraja na dunia itakusifu na kukutukuza. 'Juu' i pamoja nawe na "chini" pamoja na maadui zako. Basi usubiri mpaka siku ya ahadi ifike. Tauni itafikiwa na wakati ambapo yeyote hatashikwa nayo, yaani mwisho ni mwema.<sup>11</sup> Sasa kwa wahyi huu mambo matatu yamethibitika (1) Ya kwanza, tauni imekuja duniani kwa sababu Masihi Mau'udi wa Mungu si tu alikataliwa bali alipewa udhia, akafanyiwa njama za kumwua, alitwa kafiri na dajali. Basi, Mungu Hakutaka kumwacha Mtume wake bila ushahidi, kwa hiyo Akazifanya mbingu na ardhi, zote mbili, kuwa mashahidi wa ukweli wake.

---

<sup>11</sup>Zamani, hapo kabla, Mungu Akanipasha habari kuhusu tauni hii Akidondoa maneno ya mwingine: يَا مَسِيحَ الْخَلْقِ عَدْوَانَا (Ee Masihi wa viumbe utuangalie) Lakini leo 21 Aprili 1902, ufunuo huo ulifunuliwa tena hivi: يَا مَسِيحَ الْخَلْقِ عَدْوَانَا. يَا مَسِيحَ الْخَلْقِ عَدْوَانَا لَنْ تَرَى مِنْ بَعْدِ مَوَآدِنَا وَفَسَادِنَا Yaani, Ee Masihi wa Mungu uliyetumwa kwa viumbe, tuangalie haraka na tuokoe kwa maombezi yako; hutaona baadaye uchafu wetu wala hautabaki ufasidi wetu hata kidogo, yaani tutanyoka na tutaacha kutusi na kutumia midomo michafu. Maneno haya ya Mungu yanaafikiana na ufunuo huu wa Barahine Ahamadiyya kwamba katika siku za mwisho tutawapelekea watu tauni, kama Alivyosema: كَذَلِكَ مَنَّا عَلَى يُوسُفَ لِيُصْرِفَ عَنْهُ السُّوءَ وَالْفَحْشَاءَ Yaani, Tutamfanyia Yusufu huyu hisani kwa njia ya tuani kwamba Tutafumba midomo ya watu wenye midomo michafu ili wajiepushe na matusi wakihofia. Kuhusu siku hizo ndiyo maneno haya ya Mungu ambamo nikaarifiwa kuhusu kauli ya ardhi ambayo ndiyo hii: يَا رَبِّي اللَّهُ كُنْتُ لَا أَعْرِفُكَ Yaani, Ee walii wa Mungu, nilikuwa sikutambui hapo kabla. Maelezo yake ni haya kwamba katika kashfi ardhi ililetwa mbele yangu, nayo ikanena hivi kwamba mimi nilikuwa sikujui mpaka sasa kwamba u walii wa Rahmani. (Mwandishi)

Mbingu ilitoa ushahidi kwa jua na mwezi kupatwa katika Ramadhani, na ardhi ilitoa ushahidi kwa tauni ili yatimie naneno ya Mungu yiliyomo katika *Barahine Ahmadiyya*, nayo ndiyo haya:

قُلْ عِنْدِي شَهَادَةٌ مِنَ اللَّهِ فَهَلْ أَنْتُمْ تُؤْمِنُونَ. قُلْ عِنْدِي شَهَادَةٌ مِنَ اللَّهِ فَهَلْ أَنْتُمْ تُسَلِّمُونَ

Yaani, ninao ushahidi wa Mungu, je, mtaamini au la? Nasema tena kwamba ninao ushahidi wa Mungu, basi je, mtakubali au la? Maana ya ushahidi wa kwanza ni ushahidi wa mbinguni ambamo hamna karaha, kwa hiyo hapo neno *Tuminun* (mtaamini) limetumiwa. Na ushahidi wa pili ni wa ardhi, yaani wa tauni, ambamo mna karaha, kwani kwa kuhofisha inaingiza katika Jumuiya hii, hivyo hapo neno *Tuslimun* (mtakubali) limetumiwa. (2) Jambo la pili lililothibitika katika wahyi huu ni kwamba tauni hii itaondoka pindi watu watakapomkubali aliyetumwa na Mungu, na kwa akali watakapoachana na fitina na udhia na midomo michafu. Kwani, katika *Barahine Ahmadiyya* Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Nitatuma tauni katika siku za mwisho ili Nifumbe midomo ya mahabithi na wafitini wanaomtusi Mtume Wangu. Hakika yenyewe ni kwamba kumkataa tu pekee mtume haku sababishi maangamizo kuletwa duniani; bali kama watu wawakatae Mitume wa Mungu kwa uungwana na ustaarabu na wasitumie nguvu wala midomo michafu, hapo adhabu yao wamewekewa huko kiama. Tauni iliyopelekwa duniani kwa

kuwasaidia Mitume haikuwa kwa sababu ya kukataa tu, bali ndiyo adhabu kwa sababu ya kufitinisha. Hivyo, sasa pia watu watakapoacha midomo michafu, dhuluma, ujeuri na uhabithi wao, na kushika mwenendo wa kiungwana ndipo onyo hili litaondolewa. Lakini wakati huo wengi wenye bahati njema watamkubali Mtume wa Mungu na watapata sehemu ya baraka za kimbinguni, na ardhi, itajaa wenye bahati nzuri. (3) Jambo la tatu lililothibitika katika wahyi huu ni kwamba katika kila hali, maadamu tauni ipo duniani, hata kama iwepo kwa miaka sabini, Mwenyezi Mungu Atahifadhi Qadian katika maangamizo yake ya kuogofya, kwani hapa ni makao makuu ya Mtume wake na ndiyo ishara kwa nyimati zote.

Sasa kama mtu akimkataa Mtume huyu na ishara hii na kufikiria kwamba kwa sababu ya sala na maombi ya kimazoea au kwa kumwabudu Yesu au ng'ombe au kwa kuamini Maveda, tauni yaweza kuondoka huku akimpinga Mtume huyu na kumhasimu na kumwasi, basi fikira hii haiwezi kupokelewa bila uthibitisho. Basi, mtu anayetaka kuhakikisha ukweli wa dhehebu lake miongoni mwa madhehebu hayo yote, anayo sasa nafasi hii nzuri sana. Kana kwamba kutoka kwa Mungu, umeandaliwa uwanja wa maonyesho kwa kutambua ukweli au uongo wa madhehebu yote. Na Mungu Akitangulia Amekwisha taja kwanza jina la Qadian kwa upande wake. Sasa

kama Waaria wakiona Veda kuwa kitabu cha Mungu kweli, basi wanapaswa kutoa utabiri kuhusu Banaras ambayo ndiyo makao makuu ya kufundisha Veda kwamba Mungu wao atailinda Banaras na tauni. Na wafuasi wa dhehbu la Sanatan wanapaswa kwamba kuhusu mji wowote ambako kuna ng'ombe wengi, kwa mfano kuhusu Amritsar, watabiri kwamba kwa sababu ya ng'ombe tauni haitaingia humo. Kama ng'ombe aonyeshe mwujiza wake kiasi hicho basi si ajabu serikali ikamsamehe uhai wake mnyama huyo wa kimwujiza. Kadhalika Wakristo nao wanapaswa watabiri kuhusu Kalkata kwamba tauni haitatokea humo, kwani Askofu Mkuu wa India ya Uingereza anaishi Kalkata. Halikadhalika Mian Shamsuddin na wanachama wa Anjuman Himayati Islam wanapaswa watoe utabiri kuhusu Lahore kwamba itahifadhiwa katika tauni. Munshi Ilahi Bakhsh mhasibu anayedai kupata funuo, naye ana nafasi hii nzuri kwamba kwa ufunuo wake akitabiri kuhusu Lahore, aisaidie Anjuman Himayati Islam. Na inafaa Sheikh Abdul Jabbar na Sheikh Abdul Haq watoe bishara kuhusu mji wa Amritsar. Na kwa kuwa chanzo hasa cha dhehebu la Mawahabi ni Delhi, hivyo yafaa Sheikh Nadhir Husain na Sheikh Muhammad Husain waitolee Delhi bishara kwamba haitaingiliwa na tauni. Basi, kwa njia hii mkoa mzima wa Panjab utahifadhiwa katika maradhi yaangamizayo. Na serikali nayo wajibu wake utatimilika pasipo kufanya

chochote. Na kama watu hao hawatafanya hivyo, basi itaeleweka kwamba Mungu wa kweli ndiye Yule Aliyemtuma Mtume wake katika Qadian.

Na hatimaye ikumbukwe kwamba kama watu hao wote ambao baina yao wapo Waislamu wadaio kufunuliwa ufunuo, na Mapandati wa Waaria, na Mapadre wa Wakristo, wakinyamaza kimya basi itathibitika kwamba hao wote ni waongo, na siku itawadia ambapo Qadian ikiangaza kama jua itadhihirisha kwamba haya ndiyo makao ya mkweli. Mwishowe, Mian Shamsuddin akumbuke kwamba aya: <sup>12</sup> **أَمْ مَنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ** aliyoandika katika tangazo lake na kwa hiyo akatumai kupokelewa dua, tumaini hilo si sahihi, kwani katika kauli ya Munug 'Mudh-tar' linamaanisha waliodhikika kwa kujaribiwa si kwa kuadhibiwa. Lakini wanaosumbuliwa kwa njia ya kuadhibiwa hawahusikani na aya hii, waila hakuna budi maombi ya watu wa Nuhu, na watu wa Luti na watu wa Firauni na wengine katika wakati wa kubanwa na shida yangelikubaliwa; lakini haikuwa hivyo, na Mkono wa Mungu Ukayahilikisha mataifa hayo. Na kama Mian Shamsuddin akiuliza aya gani tena yaafikiana na hali yao, basi twasema kwamba aya hii ndiyo sawa na hali yao:

<sup>13</sup> **مَا دَعَوْا الْكُفْرَيْنَ إِلَّا فِي صَلَاتٍ**

---

<sup>12</sup> Au ni nani anayemjibu aliyedhikika. (An-Naml:63)

<sup>13</sup> Lakini maombi ya makafiri hayawi ila kupotea bure. (Al-Mumin:51)

Na kwa kuwa inawezekana baadhi ya wapumbavu wakosee kuelewa lengo lenyewe la tangazo hili, kwa hiyo tunakariri tena kueleza jukumu letu la mwito, nalo ndilo hili kwamba tauni hii inayoenea nchini siyo kwa sababu nyingine yoyote ila kwa sababu moja tu, nayo ndiyo kwamba watu wamekataa kumwamini huyu aliyekuwa ameahidiwa na Mungu aliyedhihiri sawa na utabiri wa Manabii wote katika elfu ya saba ya dunia. Na watu sio tu wamemkataa bali wakamtukana Masihi huyu wa Mungu, wakamwita kafiri, wakataka kumwua, na chochote walichotaka wakamfanyia. Kwa hiyo, ghera ya Mungu ilitaka kuwateremshia onyo kwa sababu ya fitina yao na utovu wa adabu. Na Mungu Alikuwa Ametoa habari katika maandiko matakatifu ya zamani kwamba Masihi atakapodhihiri, tauni kali itazuka nchini katika siku zile kwa sababu ya watu kukataa, basi ililazimika tauni kuzuka. Na tauni iliitwa tauni kwani ndiyo jawabu kwa wenye kushutumu, na katika wana wa Israeli hiyo ilikuwa ikizuka sikuzote katika wakati wa kushutumu. Na maana ya tauni katika lugha ya Kiarabu ni mwenye kushutumu sana. Hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba tauni hii haizuki mwanzoni mwa kushutumu, bali huzuka ambapo Mjumbe na Mtume wa Mungu anasumbuliwa kupita kiasi na kudharauliwa. Basi, Enye wapenzi, hiyo haina dawa yoyote isipokuwa tu kumkubali Masihi huyu kwa moyo wa kweli na kwa ikhlasi.

Hiyo ndiyo tiba ya yakini. Na tiba ya daraja la chini ni kwamba midomo ifumbwe isipate kumkataa yeye, na ulimi uzuiliwe kutamka machafu, na adhama yake iwekwe moyoni. Nasema kweli kabisa kwamba wakati unakuja, bali upo karibu, ambapo watu watanikimbilia wakisema: "Ya Masihal-khalki adwana". Hayo niliyotaja ni maneno ya Mungu, yanayomaanisha kwamba Ewe uliyetumwa ukiwa Masihi kwa viumbe, tufanyie maombezi kuondoa ugonjwa huu wa kuangamiza. Mwelewe kwa yakini kwamba leo hamna mwombezi yeyote minghairi ya Masihi huyu isipokuwa Mtume Mtukufu<sup>sa</sup> na mwombezi huyu si mbali na Mtume Mtukufu<sup>sa</sup> bali maombezi yake kwa hakika ndiyo maombezi ya Mtume Mtukufu<sup>sa</sup> Enyi wahubiri wa Kikristo! sasa msiseme Yesu ni Rabi wetu. Na angalieni kwamba yupo kati yenu leo aliye mbora kuliko Masihi<sup>as</sup> yule. Na enyi Mashia! msing'ang'anie kwamba Husain<sup>ra</sup> ndiye mwokozi wenu, kwani nasema kweli kabisa kwamba leo yupo kati yenu aliye mbora kuliko Husain<sup>ra</sup> Na kama nasema hayo kutoka kwangu, basi mimi ni mwongo. Lakini kama nina ushahidi wa Mungu kwa hayo, basi msishindane na Mungu, isije mkawa wenye kupigana naye. Nikimbilieni sasa, kwani bado upo wakati. Yule mtu anayenikimbilia hivi sasa, namshabihisha na yule ambaye amepanda jahazi wakati hasa wa tufani. Lakini mtu asiyeniamini naona anajitupa mwenyewe katika tofani, na hana

chochote cha kujilinda nacho. Mwombezi wa kweli ni mimi niliye kivuli cha yule Mwombezi Mkuu, na dhili ya yule ambaye wapofu wa zama hizi hawakumkubali na wakamdharau sana, yaani Hadhrat Muhammad Mteule<sup>sa</sup>. Kwa hiyo, wakati huu Mungu Akajilipiza kwa Mapadre kisasi cha dhambi hili kwa neno moja tu, kwani wahubiri wa Kikristo walimfanya Isa mwana wa Mariamu kuwa Mungu na wakamtusi Sayyidna na Bawana wetu, Mkombozi wa kweli, na kwa vitabu vya lugha chafu wakaichafua ardhi, hivyo badala ya Masihi yule aliyelitwa Mungu, Mungu alimtuma Masihi Aliyehidiwa kutoka katika umati huu aliyempita sana Masihi huyo wa kwanza katika shani yake yote. Na Akamwita Masihi huyu wa pili kwa jina la Ghulam Ahmad<sup>14</sup>, ili iwe ishara kwamba Masihi wa Wakristo ni Mungu wa namna gani ambaye hawezi kukabiliana na mtumishi wa kawaida wa Ahmad<sup>sa</sup>, yaani yu Masihi wa aina gani ambaye ni mdogo sana kuliko hata mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup> katika daraja lake la kumkurubia Mungu na la kuweza kufanya maombezi. Enyi wapenzi, hilo lisiwakasirishe. Kama huyu mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup> ambaye ametumwa kuwa Masihi Aliyehidiwa, hammwoni kuwa mkubwa zaidi kuliko yule Masihi wa kwanza na mnamfanya huyo kuwa mwombezi na mwokozi, basi leteni sasa uthibitisho wa madai yenu

---

<sup>14</sup> Ghulam Ahmad maana yake ni Mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup> (Mfasiri)

haya. Na kama vile kumhusu mtumishi huyu wa Ahmad<sup>sa</sup> Mungu Alivyosema: **إِنَّهُ أَوَى الْفِرْيَةَ لَوْلَا الْإِكْرَامُ لَهْلَكَ الْمَقَامُ** ambayo maana yake ni kwamba kwa kudhihirisha heshima ya Mwombezi yule<sup>sa</sup>, Mungu Amehifadhi kijiji hiki cha Qadian katika tauni — kama mnavyooona kwamba tangu miaka mitano sita hivi kinaendelea kuhifadhiwa — na akaongeza kusema kwamba kama nisingetaka kudhihirisha utukufu na heshima ya huyu mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup>, leo ningeleta maangamizo katika Qadian pia, ndivyo mnavyopaswa kuutaja mji mmojawapo wa Panjab<sup>15</sup> badala ya Qadian, kwamba mji huo utakingwa katika tauni kwa baraka na maombezi ya Bwana wetu Masihi ikiwa ninyi nanyi mwamwona Masihi bin Mariamu kuwa mwombezi na mwokozi wa kweli. Na msipoweza kufanya hivyo, basi fikirini kwamba mtu ambaye maombezi yake hayathibitiki katika dunia hii, atafanyaje maombezi huko akhera. Na Mian Shamsuddin azingatie kwamba tangazo lake ni bure tu, halitaleta faida yoyote iwayo. Na tiba ndiyo ile tu tuliyoandika. Akumbuke kwamba hapo kabla amekwisha fedheheka yeye na jumuiya yake mbele ya serikali ya wanadamu wakishindana nami; maana, wakaiomba serikali kumwadhibu mwandishi wa kitabu cha "*Ummahatul muminin*", nami nikawakataza kufanya hivyo. Hatimaye rai yangu

---

<sup>15</sup> Kwa mfano mtaje jina la Narowal au Batala. (Mwandishi)

ikawa sahihi. Kadhalika yale maombi pia waliyotaka hivi sasa kuipelekea serikali ya mbinguni, nayo hayafai, ni upuuzi na ni bore kabisa kama yalivyokuwa maombi ya kwanza. Kumbukumbu la kweli la maombi ni hili ambalo nimelitayarisha. Hatimaye matalazimika kulikubali hilo.

(Tafsiri ya ubeti wa Kiajemi):

*Kila anachofanya mwenye busara, anakifanya mjinga pia, lakini baada ya fedheha kubwa.*

Hapo Sheikh Ahmad Hasan wa Amroha amepata nafasi nzuri ya kushindana nasi. Tumepata kusikia kwamba yeye pia, kama masheikh wengine, anajibidiisha sana kuitetea itikadi yake ya kiushirikina ili amwokoe Hadhrat Masihi mwana wa Mariamu katika mauti kwa njia yoyote na kumfanye *Khatamul Ambiyaa* kwa kumteremsha mara ya pili. Na anaona vibaya kwamba sawa na muradi wa sura An-Noor na Hadithi ya Sahihi Bukhari, <sup>16</sup> إِمَامِكُمْ مِنْكُمْ , na kulingana na Hadithi ya Muslim <sup>17</sup> أَمَّاكُمْ مِنْكُمْ, Masihi Aliyehadiwa azaliwe katika umati huu mrehemiswa, ili badala ya Masihi wa silsila ya Musa, adhihiri Masihi wa silsila ya Muhammad<sup>sa</sup> na kuangaza shani ya unabii wa Muhammad<sup>sa</sup> duniani. Bali, Sheikh huyo anataka

---

<sup>16</sup> (Imamu wenu atakuwa kutoka miongoni mwenu)

<sup>17</sup> (Atakuwa Imamu wenu kutoka miongoni mwenu)

kama ndugu zake wengine kwamba huyo mwana wa Mariamu ambaye watu takriban milioni mia tano wakimfanya Mungu wamekwisha zama katika matope ya upotevu, ashuke tena akiweka mikono juu ya mabega ya malaika, na akionyesha onyesho jipya la Uungu, aongeze milioni mia tano wengine pamoja na milioni mia tano wa awali. Kwani wakati wa kupaa mbinguni hakuna yeyote aliyemwaona – sawa na mithali (ya kiajemi): Waongozi hawaruki bali wafuasi ndio wawarushao – lakini sasa dunia nzima itamwona akishuka pamoja na malaika, na mapadri watawakemea masheikh kwamba je, hatukusema Mungu ndiye huyo! Siku hiyo yenye nuhusi itakuwaje hali ya Islam. Je, Islam itabaki duniani?

<sup>18</sup> لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ Ni dhuluma kubwa namna gani kwamba mtu aliyezikwa huko mtaa wa Khanyar, mjini Srinagar, Kashmir, amekalishwa mbinguni kimakosa. Mungu Anaweza kufanya kila kitu isipokuwa Alichokwisha ahidi kwamba Hatafanya; lakini hawezi kwa vyovyote kumleta duniani mara ya pili yule mtu ambaye hata fitina yake ya kwanza imekwisha angamiza dunia. Hawa masheikh, marafiki wapumbavu wa Islam, wanajuaje kwamba Wakristo wamekwisha pata kusaidiwa kiasi gani na itikadi kama hizo. Sasa Mwenyezi Mungu Hataki kumpa mwana wa Mariamu adhama yoyote mpya; bali sifa

---

<sup>18</sup> Laana ya Mungu iwe juu ya waongo.

alizobandikwa Hadhrat Masihi hapo kabla nazo zilimchukiza Mungu, ndiyo maana Akalazimika kusema:

ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ<sup>19</sup>

Sasa kuangalia mbinguni kwamba lini atashuka mwana wa Mariamu toka mbinguni ni ujinga mtupu. Lakini kabla yangu wale maulamaa walioendelea kufikiria kwa kuelewa visivyo kwamba mwana wa Mariamu atakuja kutoka mbinguni, hao wanao udhuru mbele ya Mungu; haifai kuwalaumu; nia zao hazikuwa mbaya; walighafilika kibinadamu. Mungu Awasamehe, kwani hawakujaaliwa elimu, na kosa lao katika kuelewa habari hii lilikuwa kama alivyokosea Daudi<sup>as</sup> katika kuelewa habari za "mbuzi za watu". Lakini Mungu Alimpatia ufahamu mwanaye, Suleimani<sup>as</sup> kama ulivyo ufunuo huu "*Fafahamnaha Sulaimana*" (Tumemfahamisha Suleimani), katika ukurasa wa mwisho wa kitabu cha *Barahine Ahmadiyya* miaka ishirini na miwili tangu leo. Maana yake ni hii, kama inavyoonekana katika funuo za *Barahine* zilizotajwa juu, kwamba watu wanapinga wakisema kwamba je, tafsiri hii ya Kurani na Hadithi unayotoa hawakuijua masheikh na wakuu wetu wa awali, lakini wewe umepata kuifahamu? Jibu lake Mwenyezi Mungu Anatoa kwamba naam, vivyo

---

<sup>19</sup> Je wewe uliwaambia watu.

hivyo imetokea kwa hakika; lakini kutokea hivyo siyo kwamba haiwezekani. Masheikh wenu hawakuwa manabii, lakini Daudi<sup>as</sup> akiwa nabii alikosea kutoa uamuzi mmoja, na Mungu Akamfahamisha mwanaye Suleimani<sup>as</sup> njia ya kuamua barabara. Basi, huyu Suleimani aliyefanywa Masihi Mau'udi, yu mwenye haki dhidi ya wazee wenu kama nabii Suleimani<sup>as</sup>. alivyokuwa mwenye haki katika uamuzi wake huo kuliko babake Daudi<sup>as</sup>.

Na kama Sheikh Ahmad Hasan haachi kunikadhibisha, basi wakati umewadia sasa apate kutambua kwa uamuzi wa kimbinguni; yaani, kama kwa kweli ananifikiria kuwa mwongo na anadhani kwamba funuo zangu ni uzushi wa binadamu wala siyo maneno ya Mungu, basi njia rahisi ndiyo hii kwamba kama nilivyosema kwa kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

إِنَّهُ أَوَىٰ أَمْرُوهُ<sup>21</sup> yeye aandike: إِنَّهُ أَوَىٰ الْقَرْيَةَ لَوْلَا الْإِكْرَامُ لَهَلَكَ الْمَقَامُ<sup>20</sup>

Dua ya waaminio Mungu huisikia. Ni mumini wa aina gani yule mtu ambaye dua ya aliye dhidi yake inakubaliwa ambaye yeye amemwita dajali, asiye na imani na mzushi, lakini dua yake mwenyewe haipokelewi. Basi jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu Amesema, Akikubali dua yangu, kwamba nitahifadhi

---

<sup>20</sup>Bila shaka Yeye Atakilinda kijiji cha Qadian. Kama Hangekiheshimu Angekiangamiza kijiji hiki.

<sup>21</sup> Bila shaka Yeye Atalinda Amroha.

Qadian katika maangamizo haya, hususan katika maangamizo ya aina hii kwamba watu wafe ovyo kwa tauni kama mbwa hadi watu walazimike kukimbia na kutawanyika, ndivyo impasavyo Sheikh Ahmad Hasan amfanye Mungu wake kwa njia yoyote kumpokelea dua kuhusu Amroha kwamba itasalimika katika tauni. Na hivi sasa dua hii inaeleweka, kwani mpaka sasa Amroha ipo maili mia mbili mbali kutoka tauni. Lakini tauni inaendelea kuhilikisha pande zote nne za Qadian ikiwa mbali maili mbili kutoka hapa. Hili ni shindano lililo wazi sana, kwani ndani yake imo heri pia kwa watu na utambuzi vile vile wa ukweli na uwongo. Kwani, kama Sheikh Ahmad Hasan akiaga dunia baada ya kufanya shindano la kulaaniana, hapo Amroha itapata faida gani? Lakini kama kwa ajili ya Masihi wake wa mawazo tu akimfanye Mungu Akubali dua yake kwamba tauni haitatokea katika Amroha, hapo siyo tu yeye atapata ushindi, bali hiyo itakuwa hisani yake kubwa kwa Amroha nzima hata kwamba watu hawataweza kupata kuishukuru barabara. Na yafaa aeneze duniani maneno ya mubahala wa aina hii kwa njia ya tangazo lililochapishwa katika siku kumi na tano baada ya kuchapishwa kijitabu hiki, ambayo maneno yake yawe haya: Ninatoa tangazo hili dhidi ya Mirza Ghulam Ahmad ambaye amedai kuwa Masihi Mau'udi. Nami niliye mumini nikitegemea kukubaliwa dua au kwa kupata ufunuo au kuota

ndoto, natangaza kwamba Amroha lazima kabisa itahifadhiwa katika kushikwa na tauni; lakini katika Qadian maangamizo yatatokea, kwani ndiyo makao ya mzushi. Kwa tangazo hili yumkini mpaka kipupwe kijacho jambo hili litaamuliwa, au mpaka kipupwe cha pili au cha tatu. Na ingawa sasa kuanzia mwezi wa Mei, sawa na Suna ya Mungu tauni itaendelea kupungua nchini, na siku za Mungu kufunga saumu zitaendelea, lakini yatarajiwa Mungu Atafutur<sup>22</sup> tena kuanzia mwanzo wa Novemba 1902. Hapo itajulikana wakati huo wa kufuturu nani na nani walishikwa na malaika wa mauti. Kwa kuwa karibu sana na makazi ya Masihi Mau'udi ni Panjab, na Wapanjabi ndio wa kwanza wanaoonekana kwa Masihi Aliyeadiwa, kwa hiyo mambo yakaanzia humu Panjab. Lakini Amroha napo si mbali na eneo la nguvu ya Masihi Aliyehidiwa, hivyo pumzi ya Masihi huyu imwuayo kafiri lazima itafika mpaka Amroha pia. Hayo ndiyo madai yetu. Kama Sheikh Ahmad Hasan baada ya kuchapisha tangazo lake atakalochapisha kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu ataweza kulinda Amroha

---

<sup>22</sup> Seyyidna Ahmad<sup>as</sup> ameeleza mahali pengine kwamba: "Hii ni wazi kwamba Mungu Hafungi wala Hafuturu. Maneno haya hayamhusu Yeye kidhahiri, maneno haya ni ya kiistiara, na yanamaanisha kwamba wakati fulani Nitaleta adhabu yangu na wakati mwingine Nitatoa amani na raha. Vitabu vya dini vimejaa istiara za aina hii. Kwa mfano, katika Hadithi imesemwa kwamba siku ya Kiama Mungu Atasema Nilikuwa mgonjwa, Nilikuwa na njaa na Nilikuwa uchi, na kadhalika." (Hakikatul Wahyi uk. 104) (Mafsiri)

katika tauni, na kwa akali vipupwe vitatu vikapita kwa amani, hapo mimi sikutumwa na Mungu. Uamuzi gani utakuwa sahihi zaidi ya huo. Na mimi nami nasema kwa kuapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba mimi ndimi Masihi Mau'udi na ndimi yule ambaye manabii waliahidi ujaji wake, na kunihusu mimi na zama zangu utabiri umo katika Torati, Injili na Kurani Tukufu kwamba wakati ule mbinguni jua na mwezi zitapatwa, na ardhini tauni kali itaenea. Na ishara yangu ndiyo hii kwamba kila mpinzani hata akikaa huko Amroha au Amritsar au Delhi au Kalkata au Lahore au Golra au Batala, kama atasema kwa kuapa kwamba mahali pake fulani patasalimika na tauni, basi lazima kabisa mahali hapo patashikwa na tauni, kwani amekosa adabu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hilo halimhusu Sheikh Ahmad Hasan pekee, bali sasa wakati wa kushindana na watu wote kutoka mbinguni umekwishafika tayari. Watu wote wanaonifikiria kuwa mwongo, kama vile Sheikh Muhammad Husain wa Batala ambaye anajulikana kama Maulawii, na Pir Mehr Ali shah wa Golra ambaye amewazuia wengi wasifuata njia ya Mungu, na Abdul Jabbar na Abdul Haki na Abdul Wahid wa Ghazni ambaye katika kundi la Maulawii Abdullah anaitwa mwenye kufunuliwa funuo, na Munshi Ilahi Bakhsh mhasibu ambaye dhidi yangu akidai kupata ufunuo amemfanya Maulawii Abdullah kuwa Sharifu na hakuchukia kusema uwongo mtupu kabisa, na

kadhalika Nadhir Husain wa Delhi ambaye ni dhalimu kitabia na ndiye wa kwanza kunikufurisha, hao wote wanapaswa kwamba katika hali kama hii walinde heshima ya funuo zao na imani yao, na watangaze kuhusu makazi yao kwamba yatalindwa katika tauni. Katika hiyo imo heri tupu kwa watu na huruma kwa serikali, tena utukufu wa hao watu utathibitka na watahesabiwa mawalii; la sivyo, watapiga muhuri juu ya kuwa kwao waongo na wazushi. Nasi karibuni, Mungu Akipenda, tutatoa tangazo moja kwa kirefu kuhusu jambo hili. Amani iwe juu ya mwenye kufuata mwongozo.

# Habari kwa watu wote wa Jumuiya yangu nzima

Kumhusu mtu mmoja mkazi wa Jammu,

jina lake Charagh Din.

Kwa kuwa mtu huyo akidai kuiunga mkono Jumuiya yetu na kujieleza kwamba mimi ni miongoni mwa dhehebu la Ahmadiyya niliyekwisha fanya baiati, ametoa tangazo moja au mawili kuhusu tauni, nami nilisikia sehemu yake fulani kwa haraka na ilikuwa haijasikilizwa ile sehemu ya kuchukiza, kwa hiyo niliidhinisha kwamba hakuna shida lichapishwe. Lakini ni sikitiko kwamba baadhi ya maneno ya hatari na madai ya ovyo yaliyoandikwa ukingoni mwa tangazo sikuweza kuyasikia kwa sababu ya watu wengi na fikara nyingine, na likaidhinishwa kuchapwa kwa dhana njema tu. Sasa makala mengine ya mtu huyu Charagh Din yaliposomwa usiku, ikajulikana kwamba makala hayo yana hatari sana na ni yenye sumu na yenye kuidhuru Islam, na yamejaa mambo ya kipuuzi na batili tangu mwanzo hadi mwisho. Imeandikwa humo kwamba mimi ni Mtume, tena Mtume imara. Na ameandika kazi yake ndiyo kuwasuluhisha Wakristo na Waislamu na kuondoa

hitilafu baina ya Kurani na Injili, na kutoa huduma hiyo akiwa mwanafunzi wa mwana wa Mariamu akaitwe mtume. Na kila mtu ajua kwamba Kurani Tukufu haikudai kamwe kwamba itapatana na Injili au Taurati, bali ikasema kwamba vitabu hivyo vimegeuzwa na kubadilishwa maneno, na ni vipungufu na visivyokamilika, na ikajiwekea taji mahususi la:

23 أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ

Na ni imani yetu kwamba vitabu hivi vyote, Injili na Torati, si chochote mbele ya Kurani Tukufu na ni vipungufu, vimegeuzwa maneno na kubadilishwa, na heri zote zimo katika Kurani, kama ulivyo ufunuo katika *Barahine Ahmadiyya* tangu miaka ishirini na miwili iliyopita:

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهُ وَاحِدٌ وَالْخَيْرُ كُلُّهُ فِي الْقُرْآنِ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ

Tazameni *Barahine Ahmadiyya* uk. 511

Yaani waambie kwamba mimi ni binadamu kama nyinyi; ninafunuliwa kwamba Mungu ni Mmoja, hakuna aliye sawa naye na heri zote zimo katika Kurani. Watu wenye mioyo safi wanaelewa hakika yake. Basi tukiacha Kurani tujitafutie kitabu gani kingine, na tukichukuliaje hiyo kwamba si kamili. Tuliyoambiwa na Mungu ni kwamba dini ya Kikristo imejifia kabisa, na Injili ni maneno yaliyokufa na

---

<sup>23</sup> Al-Maida:4

yasiyokamilika. Basi kilicho hai chalinganaje na kilichokufa? Hatupatani na dini ya Kikristo, hiyo yote ni mbovu na batili. Na leo chini ya mbingu hakuna Kitabu kingine ila Kurani Tukufu. Miaka ishirini na miwili hapo kabla ndani ya *Barahine Ahmadiyya* mliandikwa ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kunihusu mimi ambao mtaukuta katika ukurasa wake wa 241, nao ndio huu:

وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ وَخَرَقُوا لَهُ بَنِينَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ . قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ . اللَّهُ الصَّمَدُ . لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ . وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ .  
الْفِتْنَةُ هَهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ . وَقُلْ رَبِّ اذْخِلْنِيْ مُدْخَلَ صِدْقٍ

Yaani suluhu haitapatikana baina yako na Mayahudi na Wakristo, nao hawatakuwa radhi juu yako kamwe (mradi wa Nasara ni Mapadri na wasaidizi wa Mainjili). Na kisha akasema kwamba watu hao wamempangia Mungu wana na mabinti kwa mawazo yao pasipo haki, na hawajui kwamba mwana wa Mariamu alikuwa mtu mnyonge. Mungu Akipenda, Aweza kumwumba mtu mwingine mfano wa Isa mwana wa Mariamu au mbora kuliko yeye kama alivyokwishaifanya. Lakini Mungu ndiye Mmoja, Hana mshirika, ambaye Ameepukana na kufa na kuzaliwa, wala Hana aliye sawa naye! Hiyo inaashiria kwenye jambo hili kwamba Wakristo walikuwa wakipiga makelele kwamba Yesu pia hana mshirika kutokana na ukaribu wake (na Mungu) na heshima yake; sasa Mungu Asema angalieni nitamwumba

mfano wake aliye mbore hata kuliko yeye, naye ndiye Ghulam Ahmad yaani mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup>

(Tafsiri ya Shairi la Kiurdu)

1. *Kikombe cha (huba ya) Ahmad chahuisha; ni la kupendeza lililoje jina hili Ahmad<sup>sa</sup>.*
2. *Wawepo hata malaki ya manabii, lakini, Wallahi, daraja la Ahmad<sup>sa</sup>. lawapita wote.*
3. *Tumelila tunda kutoka katika kiunga cha Ahmad<sup>sa</sup>; bustani yangu ni maneno ya Ahmad<sup>sa</sup>*
4. *Acheni habari za mwana wa Mariamu<sup>as</sup>, mbora kuliko huyo ndiye mtumishi wa Ahmad<sup>sa</sup>*

Hayo si mambo ya kishairi, bali ndiyo hakika kabisa. Na kama kwa kitendo msaada wa Mungu usiwe pamoja nami zaidi kuliko Masihi mwana wa Mariamu<sup>as</sup>, hapo mimi ni mwongo. Mungu Amefanya hivi si kwa ajili yangu mimi bali kwa ajili ya Mtume wake aliyedhulumiwa. Tafsiri iliyobaki ya ufunuo huo ndiyo hii kwamba Wakristo watafanya hila kwa kuudhi, na Mungu pia Atafanya hila na siku zile zitakuwa za jaribio. Na useme: Ee Mungu, nipatie mahali katika ardhi takatifu. Huku ni kuhajiri kiroho; na nielewavyo mpaka sasa maana yake ni kwamba hatimaye badiliko litatokea ardhini, na ardhi itang'aa kwa nuru ya ukweli na haki. Sasa angalieni kwamba umbali ulio baina yetu na Wakristo ndio ulio baina ya mashariki na magharibi. Yule mtakatifu ambaye

tunamwona kuwa mbora wa viumbe vyote, hao wanamhesabia mzushi. Suluhu hupatikana katika hali ambapo makundi yote mawili yawe tayari kuacha baadhi ya itikadi zao. Lakini katika hali ambapo dini yetu na kitabu chetu kinaiona dini ya Kikristo kuwa chafu na najisi kabisa — na kwa hakika ndivyo ilivyo — basi tufanyeje suluhu? Matokeo ya hitilafu ya kidini kiasi hiki siyo suluhu kabisa, bali mwisho wake ni kwamba dini batili itaangamia kabisa, na watu wote wema katika ardhi watakubali ukweli, ndipo dunia hii itakwisha. Hatuungani hata kidogo na Wakristo kidini. Bali jibu letu kwa hao watu ndilo hili:

<sup>24</sup> قُلْ يَا أَيُّهَا الْكٰفِرُونَ ﴿١﴾ لَا اَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾

Basi ni utume mchafu namna gani huu alioidai Charagh Din. Na ni mahali pa ghera kwamba mtu akijiita mfuasi wangu atamke maneno haya machafu kwamba mimi ni Mtume kutoka kwa Masihi mwana wa Mariamu ili nisuluhishe dini hizi mbili.

<sup>25</sup> لَعْنَةُ اللّٰهِ عَلَى الْكٰفِرِينَ ﴿١﴾

Ukristo ni dini ambayo kuihusu hiyo Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu kwamba ni karibu ardhi ipasuke kwa uovu wake na mbingu zitatuke. Je, wataka suluhu nayo? Tena juu ya kuwa na akili isiyokamilika na utambuzi usiotimilika na

---

<sup>24</sup> Sema: Enyi makafiri! siabudu mnachoabudu. (Al-Kafirun:2-3)

<sup>25</sup> Laana ya Mungu iwe juu ya makafiri. (Al-Bakara:90)

utakaso usio mkamilifu kusema pia kwamba mimi ni Mtume wa Mungu, ni kuiondolea heshima namna gani Jumuiya tukufu ya Mungu, kana kwamba utume na unabii ni mchezo wa watoto. Kwa sababu ya ujinga haelewi kwamba ingawa katika zama za awali walikuwepo mitume wengine pia ili kuwasaidia baadhi ya mitume katika zama zao kama vile Haruni<sup>as</sup> pamoja na Hadhrat Musa<sup>as</sup>, lakini *Khatamul Ambiyaa* na *Khatamul Auliyaa* hawahusikani na kawaida hii. Na kama ambavyo pamoja na Mtume<sup>sa</sup> hakuwepo Mjumbe na Mtume mwingine yeyote, na masahaba wote walikuwa wafuasi wa mwongozi mmoja tu, ndivyo ilivyo hapa pia, wote ni wafuasi wa mwongozi mmoja tu; yeyote hana haki ya kuitwa Mtume – Mungu Apishe mbali.

Na kuja kwangu si pamoja na malaika wawili tu bali ni pamoja na maelfu ya malaika. Na mbele ya Mungu, wale watu wanastahili kusifiwa ambao wanashughulikia kunisaidia tangu miaka mingi, na mbele yangu na mbele ya Mungu msaada wao umekwisha thibitika. Lakini Charagh Din amesaidia nini? Ni mamoja tu awepo, asiwepo. Utaratibu huu unaendelea tangu miaka thelathini takriban, lakini yeye amezalika tangu miezi michache tu. Mimi siwezi hata kumtambua sura yake kwamba yu nani, wala hakukaa nasi, wala sijui katika jambo gani anataka kunisaidia. Je, katika mwujiza wa kuandika Kiarabu au katika kueleza elimu za ndani za Kurani

atakuwa msaidizi wangu, au katika mijadala ile migumu atanisaidia ambayo inafanywa na Wakristo na madhehebu mengine kwa kuzingatia kanuni za maumbile na falsafa? Mimi najua huyo hajui lolote la nyanja hizi zote, na nafsi inayoamrisha sana kutenda maovu imemshawishi kufanya kosa la kujisifu. Basi, kuanzia tarehe ya leo yeye ameondolewa katika Jumuiya yetu mpaka atoe tangazo la toba yake kinaganaga na atengane kwa kudumu na madai ya utume huo mchafu.

Ni sikitiko kwamba kwa majisifu yake amewaaibisha bila sababu wasaidizi wetu wakweli, na akaifahamu Islam kuwa na daraja moja sawa na dini inukayo ya Wakristo. Basi hatumjali mtu wa aina hii; watu kama hao hawawezi kutudhuru wala hawawezi kutunufaisha. Jumuiya yetu inapaswa kujiepusha kabisa na mtu wa aina hii. Sikuwa na habari kamili ya maandiko yake, kwa hiyo nikaidhini kuyachapisha; sasa maandishi ya aina hiyo yapasa kuchanwa.

Amani iwe kwa aufuataye mwongozo.

Mtangazaji,

Mnyenyekevu

Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian,

Aprili 23, 1902.

## Nyongeza nambari I

Kumhusu Charagh Din nilipokuwa ninaandika madhumuni haya, mara nikapata hali iliyo baina ya kulala na kuamka na nikafunuliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Jalali ufunuo huu: نَزَلَ بِهِ جَبْرِيلُ  
Yaani, *Jabiz* ilimshukia, naye akaifikiria kuwa ufunuo na ruya. *Jabiz* kwa hakika ni chapati iliyokauka isiyo na ladha yoyote, ambamo hamna utamu wowote inayoweza kumezwa kwa shida. Na mtu bahili na mwenye kulaumiwa pia anaitwa *Jabiz*, ambaye kitabia ana sehemu kubwa ya uchoyo, unyonge na ubahili. Na hapa neno *Jabiz* lamaanisha hadithi zile za nafsi na ndoto zilizovurugika ambazo hazina pamoja nazo nuru ya kimbinguni, na alama za ubahili zipo. Na fikira za aina hiyo ni matokeo ya jitihada kavu au ufunuo wa shetani wakati wa tumaini na uchu; au kwa sababu ya ukavu wa ubongo na kwa majimaji yale ya nyongo wakati wa kutamani kupata ufunuo. Fikira za aina hiyo zinatiliwa moyoni wakati wa kutamani kupata ufunuo. Na kwa kukosekana hali ya kiroho ndani yake fikira za aina hiyo zinaitwa *Jabiz* katika istilahi ya Mungu. Na tiba yake ni toba, kuomba ghofira na kujiepusha kabisa na fikira za aina hiyo. Waila wingi wa *Jabiz* huhatarisha kuleta wazimu. Mungu Amlinde kila mmoja na balaa hili. (Mwandishi)

## Nyongeza nambari II

Usiku, wakati hasa wa kupatwa mwezi, nilifunuliwa kuhusu Charagh Din ufunuo huu: **إِنِّي أُذِيبُ مَنْ يُرِيبُ** Mimi nitamwangamiza, Nitamhulikisha, Nitamteremshia ghadhabu kama atashuku na hataamini wala hatatubia madai ya ujumbe na utume wala hatawaomba radhi wasaidizi wa Mungu ambao tangu miaka na miaka wanashughulikia kuhudumia na kusaidia, na wanakaa nami usiku na mchana. Kwani yeye amewaondolea heshima wanajumuiya wote waliohalisika kwa kujitanguliza nafsi yake juu ya hao wote, ilhali Mungu Aliwasifu hao mara kwa mara katika *Barahine Ahmadiyya* na Akasema hao ndio watanguliao, na Akasema: <sup>26</sup> **أَصْحَابُ السُّفَّةِ وَمَا أُذْرَاكَ مَا أَصْحَابُ السُّفَّةِ** Na *Jabiz* ni chapati iliyokauka isiyoweza kutafunwa, bali hiyo inavunja meno na inamezwa kwa shida na inapasua matumbo na inasababisha msokoto wa tumbo. Basi kwa neno hilo Akaeleza kwamba utume na funuo hizo za Charagh Din ni Jabiz tu na zitamhulikisha. Lakini watu wengine ambao yeye anawakebehi wanateremshiwa chakula kilichopikwa sasa hivi na wanayo sehemu kubwa ya rehema ya Mungu.

---

<sup>26</sup> Watu wa suffa. Na nini kitakujulisha watu wa suffa ni nani?

(Tafsiri ya Shairi la Kiajemi)

1. *Chakula hasa ni kitu kingine na chapati iliyokauka ni kitu tofauti. Ewe usiyejua, chapati iliyokauka haifai kuliwa.*
2. *Marafiki wanapewa chakula kizuri kwa upendo na ukarimu, lakini wasiohusika wanapatiwa vipande vya chapati iliyokauka.*
3. *Chapati iliyokauka wanawatupia mbwa pia; na chakula kizuri wanawapelekea wapenzi kwa huba.*
4. *Iachilie mbali chapati hii iliyokauka; zinduka, tumia akili; kama u mwenye akili, basi jitafutie chakula kizuri kwa hamu sana.*

(Mwandishi)